

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



“MET Opp. Maweni
Hospital,
S.L.P. 880,
47115 KIGOMA,
Barua Pepe: rbckigoma@pccb.go.tz.
TANZANIA.

www.pccb.go.tz

KIGOMA - JUNI 26, 2020

TAARIFA KWA UMMA

KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

**ASKARI POLISI JAMII MTA A WA BANGWE KIGOMA KUFIKISHWA
MAHAKAMANI KWA KOSA LA KUOMBA NA KUPOKEA RUSHWA YA
SHILINGI 40,000/=**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (**TAKUKURU**) Mkoa wa Kigoma Leo - Juni 26, 2020 itamfikisha katika Mahakama ya Wilaya ya Kigoma Mtuhumiwa **MANDELA ELIAZELI BATROMEO** (36) ambaye ni Askari-Polisi Jamii - Mtaa wa Katonga, kwa kosa la kuomba shilingi 300,000 na kupokea kiasi cha Shilingi elfu arobaini (40,000/) kutoka kwa SAMIZI MOHAMED ALLY - mteja ambaye alienda kulalamika kwake kuhusu kuvamiwa na vibaka watatu akiwa katika eneo lake la kazi Mtaa wa Katonga kata ya Bangwe.

Mtuhumiwa MANDELA ELIAZELI akiwa ni Askari Mgambo na Polisi Jamii katika Mtaa wa Bangwe, alifanikisha kukamatwa kwa mhalifu mmoja ambaye alihusika kumvamia na kumuibia fedha Bw. SAMIZI MOHAMED ALLY na kumfikisha katika kituo cha Polisi Kigoma mjini ambapo mhalifu huyo alifunguliwa taarifa (RB) nambari KIG/RB/128/2020.

Kisa cha mtuhumiwa kuomba hongo ni kuwa, mnamo tarehe **9/2/2020** majira ya saa nne usiku, mtoa taarifa alivamiwa na vibaka ambao walimjeruhi na kumwibia fedha zake katika eneo lake la kazi Mtaa wa Katonga kata ya Bangwe.

Mtoa taarifa alitoa taarifa Polisi na ilisajiliwa kwenye kitabu kama taarifa nambari **KIG/RB/128/2020**. Mtuhumiwa kama Polisi Jamii alifanikisha

kukamatwa kwa mhalifu mmoja na kumfikisha kituo cha Polisi Kigoma na wengine walitoroka ingawa baadae walifahamika kwa kuwa walitajwa na mhalifu aliyekamatwa awali.

Mzazi wa mhalifu aliyekamatwa pamoja na wazazi wa wahalifu wengine watatu (3) ambao hawakukamatwa walijitokeza na kumwomba mtoa taarifa wayamalize, kwa maana ya kuwa wafidie fedha zake zilizoibiwa pamoja na gharama za matibabu alizotumia. Baada ya majadiliano walifika malipo ya shilingi **600,000/=**. Baada ya makubaliano hayo na malipo kufanyika na kulipwa, mtoa taarifa alienda kituo cha Polisi Kigoma mjini kuomba kesi yake ifutwe kwa kuwa ameshafidiwa ipasavyo.

Hata hivyo kabla ya kuonana na Askari Polisi Jamii, Mandela (Mtuhumiwa), alidai kuwa amepewa maelekezo na Mkuu wa Kituo cha Polisi kuwa haruhusiwi kufuta malalamiko yake hadi atoe shilingi **200,000/=**, kwa ajili ya kumpa Mkuu wa Kituo cha Polisi Kigoma Mjini na vilevile atoe shilingi **100,000/=** kwa ajili ya kumpatia Askari Mpelelezi wa kesi yake.

Licha ya kufanya jitihada za kumwona Mkuu huyo wa Kituo ilishindikana kuonana na Mkuu huyo wa Kituo. Kwa hiyo mnamo tarehe 20/02/2020, mtoa taarifa aliamua kufika **TAKUKURU** kutoa taarifa ya kushawishiwa hongo ili kesi yake iweze kufutwa.

Tarehe hiyo hiyo 20/02/2020 mtego wa rushwa uliandaliwa na mtuhumiwa alitiwa nguvuni kwa kupokea hongo ya shilingi **40,000/=** kosa ambalo ni kinyume na Kif cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na11 ya Mwaka 2007.

TAKUKURU inatoa wito kwa watumishi wote wa Umma na katika sekta binafsi mkoani Kigoma, kuepuka kujihusisha na vitendo vya rushwa wakati wa kutekeleza majukumu yao ya kazi. Watumishi wote wa Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma katika mkoa wa Kigoma wanahimizwa kuacha tabia ya kuomba au kukubali kupokea manufaa yoyote kutoka kwa mtu wanayemhudumia au wanaye tarajia kumhudumia.

Ifahamike kuwa watumishi wanalipwa mishahara na Serikali ambayo inatokana na kodi za wananchi wanaowahudumia, hivyo kila mtumishi lazima

ajue kuwa anao wajibu wa kutekeleza majukumu ya mwajiri kwa uadilifu akifuata na kuzingatia sheria kanuni, taratibu na miongozo ya kazi na siyo kufanya kazi kwa misingi ya rushwa na upendeleo.

TAKUKURU Mkoa wa Kigoma haitasita kuwachukulia hatua kali za kisheria watumishi wa Umma na watu wengine wasiotaka kubadilika, na wanaoendelea kukumbatia vitendo vya rushwa.

Imetolewa na:

Nestory Gatahwa

KAIMU MKUU WA TAKUKURU (M)

KIGOMA